Nia Dhidi Ya Mungu Sehemu Ya 3

Je Una Mwogopa?

(Attitude Towards God Part 3 - Do You Fear Him?)

na

Ellis P. Forsman

Nia Dhidi Ya Mungu Sehemu Ya 3
Je Una Mwogopa?
(Attitude Towards God Part 3 - Do You Fear Him?)

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 6, 2011

Nia Dhidi Ya Mungu Sehemu Ya 3
Je Una Mwogopa?

Mdo. 9:31

Nia njema kimsingi ni nzuri.

Zab. 100:2-4, "*Mtumikieni BWANA kwa furaha; njooni mbele zake kwa kuimba; jueni kwamba BWANA ndiye Mungu; ndiye aliyetuumba na sisi tu watu wake; tu watu wake na kondoo wa malisho yake. Ingieni mlangoni mwake kwa kushukuru; nywani mwake kwa kusifu; mshukuruni mhimidini jina lake;*"

Nia njema ni mhuhimu katika umoja wa kusanyiko la mahali fulani. Talanta zote zilizoko katika dunia haziwezi zikatengeneza nia mbaya amabayo twaweza kuwa nayo. Mit. 23:7, "*Maana aonavyo nafsini mwake, ndivyo alivyo:…*"

Kwa nia njema, juhudi zetu katika kumtumikia Bwana urithiwa na hukaa katika uwepo wao kamilifu.

Fafanuzi la nia: Hali ya akili au hisia, tabia.

Kwa maneno mengine, takwa la mtu katika kitu fulani.

Kidini tunaweza kuwa na nia inayoleta baraka toka kwa Mungu, au ile inayoleta kutokupendezwa kutoka kwake.

Hebu tuangalie baadhi ya nia tunazopaswa kuwa nazo dhidi ya Mungu.

Tunapaswa kuwa na uhakika ili tuwe na nia katika maisha haya kama tunatarajia kupokea baraka zake. Moja ya vitu katika maisha haya ni ushirika mzuri na Mungu.

Moja ya vitu katika maisha haya tunayopaswa kuwa nayo ni nia kamilifu ya kumwogopa Mungu.

Kwa kuwaandikia kanisa la kwanza, Luka anasema:

Mdo. 9:31, "*Basi kanisa likapata raha katika Uyahudi wote na Galilaya na Samaria, likajengwa likiendelea na <u>kuongezeka katika kicho cha Bwana</u>, faraja ya Roho Mtakatifu.*"

Kumbuka kwamba walikuwa "*wakiongezeka katika kicho cha Bwana*"!

Katika kusanyiko la kanisa la kwanza waliimba nyimbo za sifa na kuzidi kunyenyekea mbele za Bwana. Hawakupata ugumu wo wote kati ya upendo na kuogopa.

Katika kuliandikia kanisa la Filipi, Paulo aliwaambia: Fil. 2:12, "*Basi wapendwa wangu kama vile mlivyotii siku zote, si wakati mimi nilipokuwapo tu bali sasa zaidi mimi nisipokuwapo, utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka.*"

Wazo la "*kuogopa na kutetemeka*" katika muunganiko na Mungu siyo wazo lililo maarufu leo. Watu wanapenda kusikia upendo wa Mungu, uvumilivu, na huruma. Wakati mwingine, tunapotaja huruma za Mungu, utakatifu, na haki, ambayo watu huitikia "Mungu wangu hayuko hivyo!"

Msisitizo katika upendo wa Mungu na huruma zake leo kimsingi ni matokeo ya "jehanamu, moto, na mwali wa moto" kuhubiri kuhusu kizazi kingine. Je inaweza kuwa tunakwenda katika upande mwingine? Ambapo hakuna wazo la "*kuogopa na kutetemeka*" kama inavyohusiana na Wakristo?

Hii inaweza kuwa sababu ya Wakristo wengi kusita katika huduma yao? Yaweza kuwa kwamba tumesahau ni nani wa kumwogopa kama tukiwa wakweli katika huduma yetu? Mat. 10:28, "*Msiwaogope wauuao mwili, wasiweze kuiua na roho; afadhali mwogopeni yule awezaye kuangamiza mwili na roho pia katika jehanamu.*"

Wale wanaohubiri injili ya kijamii na siyo Neno la Mungu hawana uoga wa Bwana. Paulo alisema, "*Ole wangu nisipohubiri injili.*"

Katika somo hili, natarajia kuzungumzia mambo matatu kuhusiana na nia yetu ya kumwogopa Mungu:

- Fafanua "*Uoga wa Bwana*".
- Onyesha ni kwa nini "*uoga wa Bwana*" ni muhimu kwa Wakristo.
- Pendekeza ni jinsi gani tunaweza kuwa na "*uoga wa Mungu*" pasipo kwenda pembeni au vinginevyo.

Tunaanza na…

Kufafanua "*Uoga wa Bwana*"

Neno "*uoga*" katika Kiebrania ni "YIR'AH" NA inatumika katika Agano la Kale kuelezea: uoga, ghadhabu, ubaya, au kitu cha kuogofya (kitu kinachosababisha uoga), uoga (wa Mungu), heshimu, ogopa, huruma.

Neno la Kiyunani linalomaanisha "uoga" ni "PHOBOS" {fob'-os} au "PHOBEO" {fob-eh'o}, na inatumika kuelezea: uoga, kutisha, ghadhabu, kukimbia kutoka katika hatari, swangazwa na wito.

Katika muunganiko na "uoga wa Bwana", leo mara nyingi hutafsiriwa kama "mwenyewe kutisha" au "waajabu".

Ambayo ni sawa kulingana na jinsi inavyokwenda. Lakini fafanuzi hii hakika haiendi mbali sana. Maana hata ivyo neno "kutisha" na "ajabu" inaonyesha sehemu ya "*kutetemeka*", je watu wengi hufanya muunganiko kama huu?

"*Uoga wa Bwana*" unapaswa kujumuisha sehemu ya "*kutetemeka*"! Hata Paulo anavyoonyesha katika Fil. 2:12, kwa kuunganisha "*uoga na kutetemeka*". Fil. 2:12, "*Basi, wapendwa wangu kama vile mlivyotii siku zote, si wakati mimi nilipokuwapo tu, bali sasa zaidi mimi nisipokuwapo utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka.*"

Neno la Kiyunani la "*kutetemeka*" ni "TROMOS" na humaanisha "tetemeka au tetemeka kwa uoga". Sawa na jinsi mtu anavyoweza kutetemeka mbele ya mtu anayetaka kumtoa uhai, hivyo Yesu alitufundisha kumwogopa Bwana. Mat. 10:28, "*Msiwaogope wauao mwili, wasiweze kuiua na roho; afadhali mwogopeni yule awezaye kuangamiza mwili na roho pia katika jehanam.*"

"*Uoga wa kweli unajumuisha*" unajumuisha "kutisha na kuogofya"; kuwa mwoga katika kumuudhi Mungu kwa kila njia yo yote.

Lakini pia, kutetemeka na kutikisika kama mtu akigundua kuwa amemchukiza Mungu na hajapata msamaha!

- Ebr. 10:26-27, "*Maana kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi; bali kuna kuitazamia hukumu yenye kutisha, na ukali wa moto uliotayari kuwala wao wapingao.*"

- Ebr. 10:30-31, "*Maana twamjua yeye aliyesema, kupatiliza kisasi ni juu yangu, mimi nitalipa. Na tena, Bwana atawahukumu watu wake. Ni jambo la kutisha kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai.*"

Hii ndiyo tafsiri ya aina hiyo ya uoga: phoberos 5398 {fob-er-os'} (Kiyunani) (1) uoga uliovuviwa, uoga wa kutisha, uoga wa ajabu (2) iliyoadhiwa na uoga (KJV: kutisha, ajabu).

Ifuatayo ni mfano: Ebr. 12:28-29, "*Basi kwa kuwa tunapokea ufalme usioweza kutetemeshwa, na mwe na neema ambayo kwa hiyo tumtolee Mungu ibada ya kumpendeza, pamoja na unyenyekevu na kicho; maana Mungu wetu ni moto ulao.*"

Uoga wa Mungu ni eulabeia {yoo-lab'-i-ah} kuogofya, kutisha, uoga dhidi ya Mungu, uoga wa Mungu huruma (3) kuogopa kiukweli, tisha (KJV: uoga wa Mungu. Uoga).

Dhamani ya nia kama hiyo inaonekana tunapoendelea mbele na sasa angalia…

Umuhimu wa "*uoga wa Bwana*"

Katika kitabu cha Mithali, tunajifunza kwamba…

- Mit. 1:7, "*Kumcha BWANA ni chanzo cha maarifa, bali wapumbavu hudharau hekima na adabu.*"
- Mit. 8:13, "*Kumcha BWANA ni kuchukia uovu; kiburi na majivuno, na njia mbovu, na kinywa cha ukaidi pia nakichukia.*"
- Mit. 10:27, "*Kucha BWANA kwaongeza siku za mtu; bali miaka yao wasio haki itapungua.*"
- Mit. 16:6, "*Kwa rehema na kweli uovu usafishwa; kwa kumcha BWANA watu hujiepusha na maovu.*"
- Mit. 19:23, "*Kumcha BWANA huelekea uhai; atakaa ameshiba; hatajiliwa na ubaya.*"
- Mit. 22:4, "*Thawabu ya unyenyekevu ambao ni kumcha BWANA ni utajiri na heshima, nayo ni uzima.*"

Katika vifungu hivi tunajifunza kwamba *uoga wa Bwana*"…

- Tunakaribia wenyewe katika hazina ya hekima ya Mungu na uelewa.
- Tutachukuliwa na uovu na ituharibu.
- Maisha yetu yanaweza kufupishwa kwa kukataa kwetu kusikiliza neno la Mungu (kama vile, kuteseka kwa magonjwa ya zinaa kwa sababu hatukusikiliza Neno lake juu ya uhusiano wa kimwili).
- Hatutaufikia upendo wa Mungu inayotupatia uhakika na ujasiri wa wokovu wetu.
- Tukianguka katika dhambi, hatutavutiwa na toba na kumgeukia Mungu.
- Hatutavutiwa katika kweli "*tuthibitishe wokovu wetu*"!

Pasipo "*uoga wa Bwana",* hatuwezi tu kumpendeza Mungu. Isa. 66:1-2, "*BWANA asema hivi, mbingu ni kiti changu cha enzi, na dunia ni mahali pa kuweka miguu yangu; mtanijengea nyumba ya namna gani? Na mahali pangu pa kupumzikia ni mahali gani? Maana mkono wangu ndio uliofanya hivi vyote, vitu hivi vyote vikapata kutokea, asema BWANA; lakini mtu huyu ndiye nitakaye mwangalia, mtu aliyemnyonge, mwenye roho iliyopondeka, atetemekaye asikiapo neno langu.*"

Ni yule tu "*Atetemekaye anaposikia neno Lake*" ndiye aliye na ahadi za Mungu kupata rehema zake!

Zab. 103:17-18, "*Bali fadhili za BWANA zina wamchao tangu milele hata milele, na haki yake ina wana wa wana; maana wale walishikao agano lake, na kuyakumbuka maagizo yake ili wayafanye*."

Lakini mtu anajengaje "*uoga wa Bwana uliokamili*" pasipo kwenda katika njia ya vizazi vya awali?

Kujenga "*uoga wa Bwana*"

"*Uoga wa Bwana*" huja kwa kupitia neno la Mungu, sawa na jinsi imani inavyokuja! Rum. 10:17, "*Basi imani chanzo chake ni kusikia na kusikia huja kwa neno la Kristo*."

Hii inaweza kusemwa pia kwamba kwa "*uoga wa neno la Mungu*"! Zingatia Kumb. 31:10-13, "*Musa akawaamuru, akasema mwisho wa kila mwaka wa saba, wakati wa maachilio wakati ulioamriwa wa sikukuu ya vibanda, Israeli wote wafikapo ili kuonekana mbele za BWANA , Mungu wako mahali pale atakapopachagua, uisome torati hii mbele ya Israeli wote masikioni mwao. Wakusanye watu, wanaume na wanawake na watoto, na mgeni wako aliyemo malangoni mwako, wapate kusikia na kujifunza, na kumcha Bwana Mungu wenu, na kuangalia kutenda maneno yote ya torati hii; na watoto wao wasiojua wapate kusikia na kujifunza kumcha BWANA Mungu wenu, siku zote mtakazokaa katika nchi mnayoivukia Yordani ili kuimiliki.*"

Mtu anaposoma neno la Mungu wanapaswa kupata kiwango cha juu chenye afya ya "*uoga wa Bwana*".

Zingatia maneno ya Paulo katika Rum. 2:4-11, "*Au waudharau wingi wa wema wake na ustahimili wake na uvumilivu wake, usijue ya kuwa wema wa Mungu wakuvuta upate kutubu? Bali kwa kadiri ya ugumu wako, na kwa moyo wako usio na toba, wajiwekea hakiba ya hasira kwa siku ile ya hasira na ufunuo wa hukumu ya haki ya Mungu, atakayemlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake wale ambao kwa saburi katika kutenda mema wanatafuta utukufu na heshima, na kutokuharibika, watapewa uzima wa milele; na wale wenye fitina wasioitii kweli, bali wakubalio dhuluma watapata hasira na ghadhabu; dhiki na shida juu ya kila nafsi ya mwanadamu atendaye uovu, Myahudi kwanza na Myunani pia; bali utukufu na amani kwa kila mtu atendaye mema, Myahudi kwanza na Myunani pia; kwa maana hakuna upendeleo kwa Mungu.*"

Wale wasiolitii neno la Bwana wana sababu ya kuogopa.

Au vipi kuhusu maneno ya Petro katika 2 Pet. 3:7-14, "*Lakini mbingu za sasa na nchi zimewekwa akiba kwa moto , kwa neno lilo hilo,*

zikilindwa hata siku ya hukumu, na ya kuangamia kwao wanadamu wasiomcha Mungu. Lakini wapenzi msilisahau neno hili, kwamba kwa Bwana siku moja ni kama miaka elfu, na miaka elfu ni kama siku moja. Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumila kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba. Lakini siku ya bwana itakuja kama mwivi; katika siku hiyo mbingu zitatoweka kwa mshindo mkuu, na viumbe vya asili vitaunguzwa na kufumuliwa na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea. Basi kwa kuwa vitu hivi vyote vitafumuliwa hivyo, imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenendo mtakatifu na utauwa, mkitazamia hata ije siku ile ya Mungu, na kuihimiza ambayo katika hiyo mbingu zitafumuliwa zikiungua, na viumbe vya asili vitateketea na kuyeyuka? Lakini kama ilivyo ahadi yake, tunatazamia mbingu mpya na nchi mpya, ambayo haki yakaa ndani yake. Basi wapenzi kwa kuwa mnatazamia mambo hayo fanyeni bidii ili mwonekane katika amani kuwa hamna mawaa wala aibu mbele yake."

Uoga wa Mungu uliokamili unatufanya tujifunze maandiko ili kwamba tuweze kuhakikishiwa kwamba maisha yetu yanampendeza.

Neno la Mungu likitumika kwa usahihi, litapata uwiano sahihi.

Hataivyo, ni muhimu kusisitiza, kwamba ili kuepuka mambo ya pembeni , lazima tusome Neno la Mungu **lote**.

Wengi wanasoma tu zile sehemu zinazofunua upendo wa Mungu na huruma, na hawana "*uoga wa Bwana.*"

Wengine wanasisitiza, vifungu vinavyozungumzia "moto, jehanamu na mwali wa moto" na hawajui upendo wa Mungu wa ukarimu.

Mtu mmoja anajenga nia au mtazamo wa kujitoa ambao unafanya utukufu wa Mungu kuwa mdogo na haki yake. Lakini wengine wanakuwa na mtazamo mbaya wanasahau rehema na huruma ya Mungu.

Hata katika kifungu tulichosoma hapo juu, mazingira ya kila kimoja inazungumza zaidi kuhusiana na neema ya Mungu na msamaha kwa wale watakaotubu!

Hivyo tunatakiwa kuwa makini jinsi tunavyolitumia neno la Mungu, lakini tunaulazima wa kulitumia!

Hitimisho

Zab. 89:7, "*Mungu huogopwa sana barazani pa watakatifu, ni wa kuhofiwa kuliko wote wanaomzunguka.*"

Kwa nini tunapaswa "*Kumwogopa Bwana*"? ili kwamba tuwe na uhakika katika "*kuhakikisha wokovu wetu kwa uoga na kutetemeka"!*

Onyo hili ni muhimu, kama ilivyoandikwa katika: Ebr. 4:1-2, "*Basi ikiwa ikaliko ahadi ya kuingia katika raha yake, na tuogope mmoja wenu asije akaonekana ameikosa. Maana ni kweli sisi nasi tumehubiriwa habari njema vile vile kama hao. Lakini neno lile lililosikiwa halikuwafaa hao, kwa sababu halikuchanganyika na imani ndani yao waliosikia.*"

Na tena, Ebr. 4:11, "*Basi na tufanye bidii kuingia katika raha ile ili kwamba mtu ye yote asije akaanguka, kwa mfano uo huo wa kuasi.*"

Wengine wananukuu 1 Yoh. 4:7-18 ili kuonyesha kwamba wanachagua kumpenda Mungu kuliko kumwogopa, "*Wapenzi na tupendane; kwa kuwa pendo latoka kwa Mungu, na kila apendaye amezaliwa na Mungu, naye anamjua Mungu. Yeye asiyependa hakumjua Mungu kwa maana Mungu ni pendo. Katika hili pendo la Mungu lilionekana kwetu kwamba Mungu amemtuma mwanawe pekee ulimwenguni ili tupate uzima kwa yeye. Hili ndilo pendo si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba yeye alitupenda sisi akamtuma mwanawe kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu. Wapenzi, ikiwa Mungu alitupenda sisi ivi, imetupasa na sisi kupendana. Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote. Tukipendana Mungu hukaa ndani yetu, na pendo lake limekamilika ndani yetu. Katika hili tunafahamu ya kuwa tunakaa ndani yake, naye ndani yetu, kwa kuwa ametushirikisha Roho wake. Na sisi tumeona na kushuhudia ya kuwa Baba amemtuma Mwana kuwa mwokozi wa ulimwengu. Kila akiriye ya kuwa Yesu ni mwana wa Mungu, Mungu hukaa ndani yake naye ndani ya Mungu. Nasi tumelifahamu pendo alilonalo Mungu kwetu sisi, na kuliamini. Mungu ni pendo naye akaaye katika pendo, hukaa ndani ya Mungu, na Mungu hukaa ndani yake. Katika hili pendo limekamilishwa kwetu, ili tuwe na ujasiri katika siku ya hukumu; kwa kuwa kama yeye alivyo; ndivyo tulivyo na sisi ulimwenguni humu. Katika pendo hamna hofu; lakini pendo lililo kamili huitupa nje hofu, kwa maana hofu ina adhabu; na mwenye hofu hakukamilishwa katika pendo.*"

Watu wanaposema wanachagua kumpenda Mungu badala ya kumwogopa wanashindwa kuelewa kifungu hiki.

Kama hakika tunampenda, tutapenda kujifunza kila kitu kumhusu yeye na neno lake, na tutapenda kufanya kila kitu katika uwezo wetu ili kumpendeza. Hivyo ndivyo tunavyomwonyesha kwamba tunampenda. Tukijifunza neno lake na kuishi kwalo kwa ubora wa uwezo wetu, uoga wa madhara yo yote zitafutwa.

Hataivyo, tukishindwa kuwa na heshima ya hali ya juu, kwake na kwa neno lake tunatarajia kupokea madhara ya kutomsikiliza. Kwa hili tunapaswa kumwogopa sana na kutetemeka. Tunapaswa kuwa na kiwango cha uoga katika maisha yetu ili kujifunza neno lake na

kuhakikisha kwamba tusije tukapatikana na hatia tukisimama mbele zake katika siku ya hukumu.

Kwa "*uoga wa Bwana*" tutaweza "*kuuthibitisha wokovu wetu*", tutafanya kazi…ili kuingia katika pumziko la [mbingu]!

2 Kor. 7:1, "*Basi wapenzi wangu kwa kuwa tuna ahadi hizo na tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukitimiza utakatifu katika kumcha Mungu.*"

Je! "*unakamilisha utakatifu katika uoga wa Mungu*"?